

## **Maandiko Yanasema Nini Kuhusu Uungu?**

Makanisa ya Kristo wanawajibu wa kufundisha ukweli kuhusu yote. Tukishindwa kufundishwa ukweli tunaelewa tutapotea, Mat. 7:21. Kwa hiyo ni wajibu wetu na mapenzi yetu kufundisha yote yaliyotoka juu kwa Baba. Na fundisho moja kati ya mengi ni fundisho kuhusu Uungu.

### **I. Tufafanue Uungu.**

- A. Neno “Uungu” limetumika mara mbili katika Biblia ya Ki-Swahili na mara tatu katika Biblia ya Ki-Ingereza (Ki-Swahili na Ki-Ingereza-Mdo. 17:29; Rum. 1:20; Ki-Ingereza Kol. 2:9). Kufuatana na kamusi ya Ki-Yunani kila mstari unatumia neno tofauti lakini maana ni sawa.
- B. Lakini ni muhimu kwa sisi tuelewa neno “Uungu” ni nafsi tatu zinafanya Mungu. Lakini wakati tunafikiri kuhusu neon “Uungu” tusifikiri kwamba kuna watu watatu. Kwa sababu ni moja tu kati ya nafsi tatu zilifika hapa ulimwenguni.
1. Yesu ambayo ni neno alivaa \_\_\_\_\_, Yon. 1:1, 7, 14.
  2. Ni Yesu tu anajulikana kuwa mwanadamu, 1 Tim. 2:5.
  3. Aliacha hali yake ya Uungu ili aje kama mwanadamu, Flp. 2:6-7.
  4. Yeye tu alikuwa na alimwaga damu kwa ajili ya wote, Flp. 2:8-11.
  5. Na yeye tu alikuwa mtu na Mungu.
  6. Soma 1 Tim. 3:16.

### **II. Nafsi tatu lakini Mungu moja.**

- A. Watu wengi siku hizi wanashindwa kuelewa jinsi Mungu alivyo. Ni kwa sababu katika hali ya mtu sisi hatuna ufahamu kama Mungu kwa hiyo kuelewa mambo ya Mungu ni vigumu. Lakini kama hatuelewi kidogo jinsi Mungu alivyo basi ni kosa la letu kwa sababu amefafanua wenyewe katika maandiko, Efe. 3:4.
- B. Biblia inatufundisha kuna Mungu moja, Efe. 4:6.
1. 1 Kor. 8:6, Kwetu kuna \_\_\_\_\_.
  2. Zek. 14:9, Bwana \_\_\_\_\_ na Jina \_\_\_\_\_.
  3. Isa. 42:8, Mungu ndiyo \_\_\_\_\_.
- C. Sasa tunatambua kuna nafsi tatu kati ya Mungu, Mat. 28:19.
1. Nafsi tatu ni \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_.
- D. Pia tunahitaji kuelewa neno “Mungu” pia ina maana “Uungu” au “Umungu”.
1. Na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanashirikiana katika hali ambayo tunafahamu ni Mungu.
  2. Wayahudi walishindwa kuelewa haya, Yn. 10:30-31; Yn. 8:58.
    - a. Kwa sababu walitaka kumuuwu Yesu alipodai yeye na Baba yake ni kitu kimoja.
    - b. Yn. 10:32-33.
    - c. Walishindwa kuelewa Uungu anaweza kuchukuwa hali ya mtu

wakati bado ana hali ya Mungu kule mbinguni.

### **III. Baba Na Mwana.**

- A. Maandiko yanaeleza sana na yanaonyesha Baba na Mwana ni nafsi mbili tofauti.
  1. Hata Yesu aliposema “Baba na Mimi ni moja”, Yn. 10:30, Mimi =1 na Baba =1 (1+1=2). Tunaona hapa nafsi mbili.
- B. Lugha ya Biblia inaongea kuhusu nafsi mbili.
  1. Mungu aliye Baba sio mwanadamu bali ni Uungu.
  2. Mungu aliye Yesu alikuwa Mungu na akavaa mwili kwa muda na akarudi mbinguni, Ebr. 10:5.
- C. Injili ya Yohana ni kitabu kizuri kinaleza Uungu.
  1. Yn. 3:16, Tuna mtoaji na yule ambaye ni zawadi. Kwa hiyo walikuwepo wawili.
  2. Yn. 3:13, Yeye aliyepanda mbinguni ni yule aliyeshushwa kutoka mbinguni, moja alikuwepo hapa ulimwenguni wakati moja alikuwepo mbinguni.
  3. Yn. 6:44-45, Moja hawezi kwenda kwa Baba asipokwenda kwa nani kwanza? \_\_\_\_\_
  4. Yn. 7:33, Yesu alikuwa aenda kwa nani? Nani alimtuma yeye? Kwa maana walikuwepo wawili!
  5. Yn. 8:16, Yesu hayupo peke yake bali upo na atahukumu na \_\_\_\_\_.
  6. Yn. 8:17-18, tunaona tena kuna nafsi mbili ambazo ni washahidi.
  7. Na kuna mistari mingi inayoleza kuwa kuna nafsi mbili, Baba na Mwana. Na wale wawili ni wamoja. Yn. 8:28, 42; 10:36; 12:27-30, 44, 49; 14:10, 15-17, 23-24, 26, 28.
  8. Mwishoni katika Yn. 16:7-13, tunaona nafsi tatu. Tunaona Baba (nafsi moja) Yesu (nafsi ya pili) na Roho Mtakatifu (nafsi ya Tatu). Kwa hiyo nafsi tatu lakini Mungu moja, Uungu.

#### **Hitimisho:**

Biblia inatufundisha kwamba Mungu ni nafsi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Kila mmoja ni nafsi tofauti. Baba sio Roho, Roho sio Yesu na Yesu sio Baba. Lakini wote wanashiriki katika Uungu au Mungu. Wote wanafanya kazi pamoja, wana nia moja, na wanaitwa Mungu.